**JAMHURI YA MUUNGALNO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**SHULE YA SEKONDARI MPEMBA,**
**S.L.P 302,**
**TUNDUMA.**
**…../…..../ 2021**

**SIMU 0769840098, 0622010996**
**KUMB.MPSS/F/V/VOL 1/**

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPEMBA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2021. (JOINING INSTRUCTIONS)

Mpendwa mwanafunzi………………………………………………………. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (HKL,HGL)…………… Mwaka 2021-2022 katika shule ya Sekondari Mpemba. Unatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe…………………..kinyume cha hapo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. **Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.**

1. **Pamoja na barua hii naambatanisha orodha ya vifaa ambavyo lazima uwe navyo**, sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakaokuwa mwanafunzi wa shule hii, fomu ya udhibitisho wa uraia wako (unaweza kuleta nakala ya cheti cha kuzaliwa), fomu ya udhibitisho wa afya yako, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla hujafika shuleni, Pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule. Kumbuka kipimo cha maendeleo yako ni taaluma, kazi za nje pamoja na nidhamu yako ndani na nje ya shule kwa muda wote utakao kuwa shuleni hapa.

   Mzazi/mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa umakini ili kuepuka usumbufu siku za baadaye.

2. **MAHALI SHULE ILIPO**: Shule ipo Mkoa wa Songwe, wilaya ya Momba, Halmashauri ya Mji Tunduma katika kata ya Mpemba.

   Unapokuja shukia kituo kidogo cha mabasi Mpemba, shule iko kilomita moja na nusu barabara iendayo wilaya ya Ileje.
   Mwanafunzi atapokelewa kama atakua.
   i. Amejaza kwa usahihi fomu kujiunga na shule hii akishirikiana na mzazi/mlezi wake.
   ii. Amepimwa afya yake katika hospitali/kituo cha afya na fomu ya request for medical examination imejazwa na Medical Officer katika hospitali au kituo cha afya cha serikali.
   iii. Amejaza taarifa binafsi kwa usahihi.
   iv. Amekamilisha maagizo yote yaliyoandikwa katika barua hii na mahitaji ya lazima ya shule (karo na michango mingine). Fomu hizo tatu muhimu zimeambatanishwa na barua hii.

Baada ya kukamilisha maagizo yote apo juu, mwanafunzi aje na fomu zilizo jazwa siku ya kwanza anaripoti. Asipokuja nazo **HATOPOKELEWA**. Mwanafunzi anatakiwa afike hapa shuleni mapema tarehe ya kufunguliwa shule.

……………………………

**MWL GONSALVA S. MBULIGWE**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE MPEMBA SEKONDARI S.L.P 302 TUNDUMA



Scanned with CamScanner

**SHERIA ZA SHULE**

Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa asijihusishe na makosa yafuatayo hapo chini vinginevyo anaweza kufukuzwa/kufutwa shule:

1. Wizi.
2. Kutohudhuria masomo bila taarifa.
3. Uasherati na Ushoga.
4. Ulevi na Matumizi ya madawa ya kulevya.
5. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake/walimu/walezi.
6. Uvutaji wa bangi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kupigana na kupiga.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
10. Kudharau Bendera ya Taifa.
11. Kuolewa au kujihusisha na mapenzi.
12. Kupata mimba, kufanya jaribio la kujiua.
13. Kutoa mimba.
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
15. Kukataa adhabu kwa makusudi.
16. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe.
17. Kulala nje ya shule bila ruhusa (Utoro).
18. Kuwasaha mshumaa bwenini/kukutwa na kiberiti.
19. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa.
20. Kumiliki/kukutwa au kutumia kifaa chochote cha mawasiliano katika mazingira ya shule.
21. Kujihusisha, kumiliki na kutumia kifaa chochote cha umeme.

**VIFAA NA MAHITAJI MENGINE**

1. Passport size nne (4), yenye rangi ya blue nyuma na avae shati la shule jeupe na picha nne tofauti za walezi/wazazi/ndugu wa karibu watakao tambulika shuleni.
2. Soksi nyeupe nzito zisizo na maua jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili visivyo na visigino virefu.
3. Mavazi mengine ni nguo za ndani za kutosha, taulo, blanketi nzito, mashuka mawili(2) moja la blue bahari(Light Blue) na jingine la pink, ya kutandika kitandani na foronya zake za mito, na sanduku imara la chuma na chandarua rangi nyeupe.
4. Mwanafunzi aje na Sweta rangi ya kijani nyeusi (Dark Green), Vitenge viwili. **(Akija na idadi ya nguo Zaidi ya hizi atalazimika kuzirudisha nyumbani kwa gharama zake)**
5. Kijiko cha kulia chakula , sahani na kikombe, ndoo ndogo moja na galoni (dumu la lita 5) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
6. Aje na:
    - Spring file moja (1) rangi ya kaki.
    - Mkebe (mathematical set), calculator kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi.
    - Madaftari makubwa 9 (Counter books three(3) quire) peni, penseli.
    - Begi la kubebea daftari.



Scanned with CamScanner

# KANUNI ZA SHULE

## A. HESHIMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutokutumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha **fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi** kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbia aliko mtu anayekuita katika mazingira ya shule.
8. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
9. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
10. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
11. Kunyosha mkono juu na usimame unapouliza au kujibu maswali.
12. Kukaa kimya wakati wote unapokuwa darasani, usitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
13. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.

## B. MAHUDHIRIO

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya madarasa.

## C. MAANDALIO JIONI

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 usiku. **Mwanafunzi haruhusiwi kukaa au kulala bwenini muda huo ukipatikana adhabu itatolewa dhidi yake.**
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.

## D. KUWAHI

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda.
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.



Scanned with CamScanner

## E. SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa

1. Masomo darasani.
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini.
5. Kwenye maandamano rasmi.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo.
7. Kazi za mikono (**vazi la kazi**)
8. Michezo.

**NB**: Mwanafunzi harusiwi kuvaa kofia, mizura, nguo fupi, zenye mipasuo, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa hereni, mkufu bangili, viatu vyenye visigino virefu, mapambo mengine yoyote pamoja na sare akiwa shuleni.

## F. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu:
   (a) Chumba cha walimu (staffroom)
   (b) Ofisi za shule
   (c) Maabara
   (d) Jikoni
   (e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

## G. UGONJWA

1. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matroni wa shule, mwalimu mlezi n.k mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitunzwe kwa matroni.
2. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika sehemu maalumu kwa kibali cha shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika hospitali ya serikali.
3. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe **uongozi wa shule au Matron wa shule, mara afikapo shuleni**.
4. Shule haitoi **CHAKULA MAALUMU (special diet)** kwa manafunzi mgonjwa.

## H. ANGALIZO KWA MWANAFUNZI

1. Mwanafunzi harusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shuleni.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano **barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k**
3. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.

Scanned with CamScanner

**MAHITAJI MUHIMU (ZILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE HAPO CHINI)**

**A. ADA NA MICHANGO**


1. Ada ya shule……………………………. Tsh 70,000/= kwa mwaka au 35,000/= kwa nusu muhula kwenye Akaunti na: **6151200008 (NMB) tafadhali andika jina la mwanafunzi na kidato kwenye pay slip**.
2. Shilingi 20,000 kwa ajili ya taaluma (kwa mwaka).
3. Shilingi 30,000 kwa ajili ya malipo ya wapishi na walinzi (kwa mwaka).
4. Shilingi 5,000 hela ya tahadhari na haitarejeshwa.
5. Shilingi 10,000 kwa ajili ya matibabu.
6. Shilingi 25,000 kwa ajili ya ukarabati wa samani.
7. Shilingi 5,000 kwa ajili ya kitambulisho cha shule.
8. Shilingi 3,000 kwa ajili ya Nembo ya shule.
9. Shilingi 20,000 kwa ajili ya mitihani ya kujipima (Mock).

Jumla Tsh 188,000/= (shilingi laki moja na elfu themanini na nane)

Michango hiyo juu ilipwe kupitia akaunti ya **NMB 6151200008** na mwanafunzi anatakiwa kuja na risiti za malipo ya Benki (**ORIGINAL PAY IN-SLIP**).

- Godoro futi 2.5 kwa sita (6x 2.5).
- Toilet paper zakutosha.
- "Ream" moja (1) za karatasi nyeupe (Photocopy paper – $A_4$) na siyo fedha.
- Sare za shule Sketi mbili za marinda Pamoja na Tai zake (Dark blue nzito na Ugoro) Mwanafunzi aje ameshona , urefu wa wa nchi nane (8) kutoka kwenye goti (angalia mchoro huo. Upana wa mkanda wa kiunoni (belt) uwe nchi mbili (2) ziwe na mfuko wa ndani upande wa kulia.

Mchoro wa Sketi mbele na nyuma




- Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu (Utanunua mwenyewe).
- T – shirts moja rangi ya bluu, iwe na kola, iwe na mfuko upande wa kushoto, isiwe na maandishi yoyote (nembo ya shule itagongwa shuleni).
- Rangi ya Ijabu ni nyeupe kwa Waislam.
- Nguo za kazi (Shamba dress) Rangi ya blue bahari mshono wa solo (angalia mchoro)





Scanned with CamScanner

- Truck suit rangi nyeusi yenye mistari mweupe pembeni isiyo bana na iliyo anchana na raba kwa ajili ya michezo (utanunua mwenyewe).
- Mfagio laini wa ndani (Soft Bloom).
- **MUHIMU MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA HATI YA MATOKEO (RESULT SLIP) YA KIDATO CHA NNE.**

## ANGALIZO KWA MZAZI AU MLEZI

1. Mzazi/Mlezi haruhusiwi kumtumia mwanao fedha nje ya utaratibu wa shule atakao ukuta mwanafunzi shuleni.
2. Mtoto akishapokelewa shuleni. Mzazi/Mlezi au ndugu yeyote haruhusiwi kuja kumuona labda uitwe na uongozi wa shule, kwa maana nyingine **"HAKUNA SIKU YA KUTEMBELEA MWANAFUNZI"**.
3. Mwanafunzi harusiwi kuja/kumiliki simu au kifaa chochote cha simu na vyakula vya aina yoyote na mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mtu wa nje ya shule yafanyike kupitia uongozi wa shule tu.
4. Mwanafunzi aripoti shuleni **akiwa amevaa sare yoyote ya shule nadhifu na yenye heshima (zisizo bana au fupi wala kuangaza)**.
5. Barua ya mwanfunzi itakayotiliwa wasiwasi itafunguliwa na uongozi wa shule.

Scanned with CamScanner

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mkoa wa ........................................................

Ofisi ya Mkuu wa wilaya,

Wilaya ya..............................

S.L.P ................................

Tarehe ..................................

Mkuu wa shule,

..............................................................................

..............................................................................

..............................................................................

## UTHIBITISHO WA URAIA WA MTANZANIA

Nadhibitisha kuwa................................................................ (jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa

Baba yake (jina kamili) ..........................................................................................

Amezaliwa katika mkoa wa ........................................ Wilaya ya ..............................................

Tarafa ya ................................................... Kata ya ............................................................

Mama yake (jina kamili) ..........................................................................................

Amezaliwa katika kata ya ......................................... Wilaya ya ..............................................

..............................................................................

Mkuu wa Wilaya

**NB**: kila mwanfunzi atalazimika kuishughlikia hati kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni. **Au leta nakala ya cheti cha kuzaliwa badala ya fomu hii.**



Scanned with CamScanner

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Mpemba Secondary School,

P.O. Box 302,

**Tunduma.**

Date: ..................................

To:

THE MEDICAL OFFICER,

.......................................................

.......................................................

.......................................................

Please examine ...........................................................................................

As to her fitness for pursuing further education at this school.

1. Haemoglobin ..........................................................................................
2. P.V. Blooding...............................................................................................................
3. (A) Blooding ............................................................................................................

(B) Hearing ........................................................................................................................

4. Blood Pressure ..............................................................................................
5. Urine for Sugar and Pregnancy tests ..........................................................................
6. Stool for routine examination ..........................................................................................
7. Asthma .....................................................................................................................
8. Skin diseases ...............................................................................................................
9. Leprosy ...........................................................................................................................
10. Pulmonary tuberculosis ..........................................................................................
11. Employs ............................................................................................................................
12. Deformity ........................................................................................................................
13. Mental problem ...............................................................................................................
14. Comments ........................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.......................................................

DESIGNATION

Scanned with CamScanner